THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2
(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

*MUDA:* ***Saa 2 dakika 30*** ***Jumatatu Novemba 10, 2003 Mchana***

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **MANNE (4),** swali moja kutoka kila sehemu.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim**

## SEHEMU A: QUR-AN

1. Andika kwa lugha ya Kiarabu Suratut-tyn (95: 1-8) kisha andika tafsiri yake kwa Kiswahili na eleza mafunzo yatokanayo na sura hiyo.

2. "Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (Hii Qur-an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda" (15:9).
Kwa mujibu wa aya ya hapo juu, eleza hatua alizochukua Mtume (s.a.w.) katika kuihifadhi Qur-an.

3. "Uteremsho wa Kitabu hiki umetoka kwa Allah mwenye nguvu na mwenye hekima." (45:2).
Kwa mujibu wa aya hii thibitisha kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah.

## SEHEMU B: TAWHIID

4. "Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Allah ni Uislamu ...." (3:19)
Kwa kutumia aya hii, eleza kwa kina kwa nini Uislamu ndiyo dini pekee iliyo ya haki mbele ya Allah (s.w.).

5. "Wanasema (kwa stihizai), je tutarudishwa katika hali yetu ya kwanza? Hata tukiwa mifupa mibovu (iliyosagikasagika).....?" (79:10-12).
Kwa kutumia ushahidi wa kihistoria, thibitisha kuwa ufufuo ni jambo jepesi kwa Allah (s.w.)

6. "Waislamu walio wengi wanajiepusha na kuabudu masanamu, makaburi, hirizi n.k. lakini bado ni washirikina wakubwa katika uendeshaji wa maisha yao ya kila siku ya kibinafsi na kijamii". Thibitisha usemi huu kwa kutumia mifano hai, ukizingatia aina kuu nne za shirk.

## SEHEMU C: FIQH

7. "Chukua sadaqa katika mali zao uwatakase kwazo na kuwataja kwa uzuri (mbele yangu) na uwaombee dua ............." (9:103)
Eleza kwa kina jinsi Zaqat na Sadaqat zinavyoitakasa mali katika Jamii ya Kiislamu.

8. Eleza umuhimu wa ndoa katika Uislamu, kisha ukiwa kama Walii wa Ramla bint Omar, mwozeshe kwa bwana Hamisi bin Shwayb.

9. "Enyi mlioamini! Mmeamrishwa kufunga kama walivyoamrishwa waliokuwa kabla yenu." (2:183).
Kwa mujibu wa aya hii, eleza namna funga inavyomuandaa muumini kuwa mcha-Mungu.

## SEHEMU D: TAREKH

10. Ukizingatia namna Mtume Muhammad (s.a.w.) alivyoandaliwa kabla ya Utume na mara tu, baada ya kupewa Utume katika Wahay wa awali, eleza mambo ya msingi ya kuzingatiwa katika harakati za kuuhuisha Uislamu katika Jamii.

11. Eleza hatua alizochukua Mtume (s.a.w.) katika kuanzisha Dola ya Kiislamu Madina kisha ainisha mafunzo yapatikanayo kutokana na hatua hizo.

12. Chambua mchango wa Waislamu katika kuianzisha Tanganyika na hatimaye Tanzania.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org